# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

### Kikao cha Kwanza - Tarehe 27 Agosti, 2013

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

*(Hapa Wabunge waliimba Wimbo wa Taifa)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge katika Mkutano wetu wa Kumi na Moja, Bunge lilipitisha Miswada mitatu ya Sheria ya Serikali iitwayo: *The Written Laws (Miscellaneous Amendment, Number two) Bill, 2013, The Appropriation Bill, 2013 and The Finance Bill, 2013.*

Kwa Taarifa hii napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kuwa Miswada hii imekwishapata kibali cha Mheshimiwa Rais na kuwa Sheria za nchi ziitwazo:-

*The Written Law (Miscellaneous Amendment) No. 2) Act, 2013,* Sheria Namba moja ya mwaka 2013*, The Appropriation Act, 2013* yaani Sheria Namba mbili ya mwaka 2013 na *The Finance Act,* 2013, Sheria Namba tatu ya mwaka 2013. Kwa hiyo, Miswada ile tuliyopitisha, sasa imekuwa Sheria.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake zilizochapishwa tangu kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu na atakayeuliza swali letu la kwanza katika Bunge hili ni Mheshimiwa Catherine Magige.

Na.1

### Kukithiri kwa Madawa ya Kulevya Nchini

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE** aliuliza:-

Biashara ya madawa ya kulevya imekuwa ikiongezeka kwa kasi hapa nchini, ambapo vijana wengi wamekuwa wakikamatwa wakiwa na madawa hayo katika viwanja vya ndege vya ndani na nje ya nchi:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza ukubwa wa biashara hiyo hapa nchini ukoje?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kuna tatizo katika ukaguzi wa abiria na mizigo katika viwanja vyetu vya ndege na inafanya juhudi gani kukabiliana na upitishwaji wa madawa haya?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa, tatizo la matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevya hapa nchini ni kubwa. Ukubwa wa tatizo hili unadhihirishwa na takwimu za ukamataji zilizokusanywa katika kipindi cha kuanzia Machi, 2000 - Machi, 2012. Katika kipindi hiki kiasi cha dawa za kulevya kilichokamatwa na jumla ya Watuhumiwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Bangi, kiasi kilichokamatwa ni tani 2,722.428 na idadi ya Watuhumiwa ni 45,470.

(ii) Mirungi, kiasi kilichokamatwa ni kilogramu 73,680.700 na idadi ya Watuhumiwa ni 4,015.

(iii) *Heroin*, kiasi kilichokamatwa ni kilogramu 873.708 na idadi ya Watuhumiwa ni 2,489.

(iv) *Cocaine*, kiasi kilichokamatwa ni kilogramu 373.5724 na idadi ya Watuhumiwa ni 836.

Mheshimiwa Spika, ukubwa wa biashara hii hapa nchini unadhihirishwa pia na idadi ya Watanzania 247 waliokamatwa kati ya mwaka 2008 hadi Julai 2013 kwa kosa la kujihusisha na dawa za kulevya katika nchi mbalimbali kama Mauritius, Falme za Kiarabu, China, Pakstani, Brazil, South Afrika na Kenya. Aidha, wageni wapatao 31 wanashikiliwa mahabusu katika Magereza ya Keko na Ukonga. Utaifa wa raia hao 31 ni Iran, Pakstani, Nigeria, Senegal na Afrika ya Kusini.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeliona tatizo lililopo katika ukaguzi wa abiria na mizigo katika viwanja vyetu vya ndege. Hatua kadhaa za kukabiliana na upitishwaji wa dawa za kulevya zimeanza kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na na kuhakikisha kuwa viwanja vyetu vya ndege vina vifaa vya kisasa kabisa vya kukagulia mizigo na abiria, kuwafukuza watumishi wasio waaminifu na wanaofanya

kazi katika viwanja vya ndege waliobainika kuhusika na kupitishwa dawa za kulevya kwa kukusudia.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Watumishi wa uwanja wa ndege waliofukuzwa hivi karibuni walishirikiana na wahusika wa madawa hayo, je, Serikali inaweza kutueleza ni akina nani hasa wanaohusika na mzigo huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa kiwango kikubwa cha madawa ya kulevya kimekuwa kikikamatwa, lakini wananchi hawaoni uwazi wa uteketezaji wa dawa hizi, je, Serikali haioni kuwa kutokuwa na uwazi wa uteketezaji wa dawa hizi kuna uwezekano mkubwa kwa watu wasio waaminifu kuyachukua tena madawa haya yaliyokamatwa na kuyauza na hivyo kuathiri juhudi za Serikali katika upambanaji wa biashara hii haramu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa hivi karibuni kuna Watumishi ambao wanafanyiwa upelelezi na wanashukiwa kuwa wamehusika au ku- *facilitate* yaani kuwezesha madawa ya kulevya kupita katika kiwanja cha ndege cha Dar es Salaam. Mamlaka zinazohusika zilichukua hatua na Mamlaka zingine zinazohusika na masuala ya Kisheria zinaendelea na upelelezi kamili ili kujua hao

waliowatuma na kujua jinsi walivyojihusisha ili wapelekwe Mahakamani na kushtakiwa.

Mheshimiwa Spika, hapa nilipo siwezi kusema ni akina nani waliowatuma kwa sababu upelelezi unaendelea ili hawa waliowatuma waweze kufikishwa kwenye vyombo vya Sheria.

Mheshimiwa Spika, la pili; ni kweli kuwa madawa yote yanayokamatwa huwekwa katika nyumba maalum na yanahifadhiwa katika maeneo yale kama vielelezo hadi kesi zinapokamilika, ni kero kubwa na ndiyo maana Serikali sasa inakuja na marekebisho ya Sheria ambayo tungependa Hati ya Mkemia Mkuu inayothibitisha kukamatwa na Madawa ya kulevya na kuthibitisha kuwa ni madawa ya kulevya ibaki kuwa ndio kielelezo cha Mahakama mpaka kesi inapokwisha ili madawa yale yanapokamatwa siku ya kwanza, yakishakaguliwa na kupewa Hati ya Mkemia Mkuu, basi yakateketezwe, kwa sababu kuna madawa yanakaa mpaka miaka kumi kutokana na kwamba kesi hazijakwisha.

Kwa hiyo, ni kero pia kwa Serikali na ndiyo maana tunachukua hatua ya kutaka kurekebisha Sheria, lakini uwazi katika uteketezaji wa madawa hayo upo, wakati wa kuteketeza madawa hayo haendi mtu mmoja kuna vyombo vyote vya ulinzi na usalama vinashuhudia uteketezaji huo. Ila ni kweli kuwa haufanywi kila mara kwa sababu dawa hizi mara nyingi tukizikamata hatuziteketezi mpaka kesi ziishe.

Mheshimiwa Spika, nataka kuwahakikishieni kuwa uwazi upo na Sheria hii tukiirekebisha uteketezaji utakuwa mara baada ya ukamataji na mara baada ya kupata hati ya Mkemia Mkuu.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa swali hili limetokea Bungeni, Serikali sasa iko tayari itakapowapata wale wahusika wakubwa waliowatuma hawa vijana kuyataja haya majina ndani ya Bunge hili? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, labda kama angesema kuwa swali hili sasa limeulizwa na siyo mara ya kwanza kuulizwa. Masuala haya ya madawa ya kulevya hayajatokea hapa Bungeni lakini yanatokea kila mara, isipokuwa ninachotaka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na inawezekana kabisa kuwa kabla hata hatujakutana Bungeni hawa watu watakuwa wametajwa na wameonekana kwenye vyombo vya Sheria , kwa sababu wanaweza wakafikishwa Mahakamani na mkawaona, mkashuhudia na mkasoma kwenye vyombo vya habari kabla ya Bunge, lakini swali lolote likiulizwa hapa, wakati wowote kama tunayo majina ya namna hiyo tutataja wala hatutasita kuwataja watu hao kwa sababu ni watu hatari na ni watu wabaya sana katika Taifa letu.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba kufahishwa na Serikali maana suala la kutajwa wauza madawa ya kulevya si la leo, watu wengi ndani ya Bunge wamesema tuna majina na Rais amesema tuna majina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona kuwa, Serikali inahangaika na kutibu wakati haitaki kuzuia na inasikitisha kuona kuwa, watu wanaobeba hiyo mizigo ndiyo wanaokamatwa wahusika hawapo. Naomba Serikali itoe kauli maana Rais ametaja na kuna baadhi ya Wabunge wametaja, hao wote wawekwe wazi na Serikali itoe kauli. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kazi ya Serikali siyo kutaja tu, kazi ya Serikali ni kuwachukulia hatua za kisheria hawa watu na Serikali haiwezi kuwachukulia hatua bila kuwa na uhakika. Orodha hizi tukiwaonesha zinazoandikwa, humu ndani tutakwisha hata humu ndani mmo wengi tu.

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Majina haya yanayotembea yako mengi sana, watu wanaandika wanavyotaka, lakini kazi ya Serikali hata tukiokota karatasi ina majina mawili milioni, tunafanya uchunguzi na wale wanaothibitika wanapelekwa kwenye vyombo vya Sheria. Kama ni kutaja tu nasema siyo jukumu la Serikali peke yake! Mbona gazeti la Jamhuri limetaja

mmeona juzi magazeti mawili yametangaza yale majina, pengine wale wana uhakika. Kama wametaja na hawana uhakika na wale waliotajwa kwenye magazeti wanaona wameonewa watakwenda Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, sisi tutaendelea kuwataja na kuwachukulia hatua watu tuliowakamata na kuwa na vielelezo sahihi vya kuwafikisha Mahakamani. Haiwezekani Serikali tukapeleka watu, wakati hatuna vielelezo, halafu tunashindwa kesi, ni aibu kwa Serikali. Lakini bado tunaomba ushirikiano wenu, ushirikiano wa raia wema ili tushirikiane kwa kasi sana kuwafichua. Mtu yeyote mwenye majina na vielelezo vya uhakika kuwa fulani anahusika na biashara haramu ya madawa ya kulevya aniletee hapa na tutamtangaza pamoja.

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**SPIKA:** Tabia ya kuzomeazomea haifai na muda umekwisha, tunaendelea na swali linalofuata ambalo litaulizwa na Mheshimiwa Suleimani Jumanne Zedi, kwa niaba yake atauliza Mheshimiwa Rage.

Na. 2

**Kuanzishwa kwa Halmashauri Mpya ya Bukene**

**MHE. ISMAIL A. RAGE (K.n.y. MHE. SELEMANI J. ZEDI)** aliuliza:-

Baraza la Ushauri la Mkoa wa Tabora *(RCC)* katika kikao cha tarehe 12 Juni, 2013 lilipitisha mapendekezo yaliyopitishwa na vikao vyote halali vya Halmashauri ya Wilaya ya Nzega na kuanzishwa kwa Halmashauri mpya ya Bukene na mapendekezo hayo kuwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

(a) Je, mapendekezo hayo yameshughulikiwa kwa kiasi gani?

(b) Je, ni lini Halmashauri mpya ya Bukene itatangazwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Jimbo la Bukene, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ilipokea mapendekezo mawili toka Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora kwa barua yenye Kumb. Na. *NDC*/L.2/13/51 ya tarehe 17 Juni, 2013. Mapendekezo hayo yanahusu:

Kwanza, kuanzishwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Bukene kunatokana na kugawanywa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega.

Pili, kufanya marekebisho ya mipaka ya Halmashauri ya Mji wa Nzega ambayo yamehusisha kuhamishwa kwa Kata mbili za Halmashauri ya Wilaya ya Nzega kwenda Halmashauri ya Mji wa Nzega. Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI imepitia mapendekezo hayo na inakusudia kutuma wataalam wake kwenda kufanya uhakiki wa mipaka ya Halmashauri ya Mji wa Nzega.

(b) Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa mchakato wa kuitangaza Halmashauri ya Mji wa Nzega, Serikali itaanza mchakato wa kuhakiki maombi ya uanzishwaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukene na kuchukua hatua muafaka.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Bukene, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina swali dogo la nyongeza. Je, katika maombi haya yaliyopitishwa na *RCC* tangu mwezi wa Sita mwaka jana, atalihakikishia vipi Bunge lako kwamba, kwa muda gani wananchi wa Bukene watapata Halmashauri yao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema kuwa, maombi yenyewe tumeyapata mwezi Juni, 2013 na wakati huo huo tunaendelea na mchakato katika Wilaya hiyo hiyo wa kuanzisha Halmashauri ya Mji wa Nzega. Kwa sasa hivi

siwezi kuwaahidi kuwa ni tarehe ngapi isipokuwa ni baada ya kukamilisha mchakato wa uanzishwaji wa Mji wa Nzega.

**MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja la nyongeza. Wilaya nyingi au Halmashauri zinazotaka kuwa Miji ni nyingi na zimepeleka maombi kwa muda mrefu, suala hili linasubiriwa na wananchi. Serikali inatamka nini na ni kwa nini Serikali isitoe program kamili ya kujua kwamba Mji fulani unafikiriwa au unategemewa kuanzishwa mwaka fulani, kuliko ilivyo sasa hivi kutangaza Miji, Mikoa lakini hatuoni taratibu za kuiendeleza kikamilifu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa kawaida kila baada ya miaka mitano ndiyo tunakuwa na utaratibu wa aidha kuongeza Mikoa, Wilaya au Halmashauri na suala la Mamlaka ya Miji Midogo tunaianzisha kwa lengo la kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanawekwa katika mipangilio mizuri.

Mheshimiwa Spika, haina maana kwamba, ukianzisha tu mamlaka ya Mji mdogo ni kwamba, kinachofuatia wakati huo huo iwe ni Halmashauri ya Mji. Lakini pale ambapo tunaona tayari ile mamlaka ya Mji Mdogo ina sifa ya kuwa Halmashauri ya Mji kwa vigezo vyote vinavyotakiwa, huwa tunaupandisha kuwa Halmashauri ya Mji lakini pia ikiambatana na maombi kutoka katika Halmashauri husika.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Ahmed Shabiby!

Na. 3

**Upungufu wa Walimu – Wilaya ya Gairo**

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS (K.n.y. MHE. AHMED M. SHABIBY)** aliuliza:-

Wilaya ya Gairo ina upungufu mkubwa wa Walimu kwa shule za Msingi na Sekondari na Walimu wapya wamepangwa katika Wilaya mbalimbali nchini mwaka huu ikiwemo Wilaya mpya ya Gairo ambayo ina Halmashauri yake:-

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuipatia Wilaya mpya ya Gairo Walimu wa kutosha ili kuziba pengo kubwa lililopo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shabiby, Mbunge wa Gairo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Gairo ni mpya iliyoanzishwa mwaka 2012/2013, kutoka Halmashauri

ya Wilaya ya Kilosa. Mwaka 2013 Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ilipangiwa Walimu wa shule za msingi 132 na wa sekondari 141. Kati ya Walimu wa Msingi 33 na Sekondari 41 walipelekwa shule zilizopo Gairo. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Gairo na Kilosa zimetengewa shilingi milioni 198.9 kwa ajili ya uhamisho ambazo zitasaidia kusawazisha Ikama ndani ya Halmashauri hizo na kuondoa mlundikano na upungufu uliokithiri katika baadhi ya maeneo ya Wilaya hizo.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali dogo moja la nyongeza. Je, ni lini pesa hiyo milioni 198 ambayo imetengwa kwa ajili ya kuwahamisha Watumishi katika kuwatenganisha katika hizi Halmashauri mbili;Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ambayo ni Halmashauri mama na Halmashauri ya Wilaya ya Gairo mpya ili kusudi watumishi wakafanye kazi ya kuwatumikia wananchi na kuleta maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya mpya ya Gairo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema ni bajeti ya mwaka 2013 na pesa zetu sasa hivi huwa zinatolewa kwa kadri zinavyokusanywa. Nina imani kabisa karibu kila robo ya mwaka watakuwa wanapata pesa hizo na kuwawezesha kuhamisha Walimu kutoka katika vituo walipo na kuwapeleka katika maeneo yenye upungufu.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona ili niulize swali moja la nyongeza. Naomba kufahamu Serikali ina kauli gani juu ya Maafisa Elimu ambao wanaacha Walimu katika shule za Mijini wakati shule za pembezoni hazina Walimu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, tayari Serikali ilishatoa kauli kwamba Walimu wagawanywe kwa mujibu wa ikama za kila shule zilizopo katika Wilaya. Tulishakataza kuwarundika katika eneo moja na kuacha maeneo ya pembezoni. Kwa kuanzia kama Serikali, zipo Wilaya za Miji mingi ambazo sasa hivi hatuzipangii tena Walimu kwa Walimu katika maeneo hayo tayari wametosheleza.

**SPIKA:** Naona swali hili limeulizwa vizuri, limejibiwa vizuri, watu watatu dakika tano. Waliouliza maswali mawili ya nyongeza nawapongeza wote. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Tunaendelea na swali linalofuata, Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Sylvester Mabumba atauliza swali hilo.

Na. 4

**Mchango wa Sekta ya Madini katika Uchumi wa Taifa**

**MHE. SYLVESTER MASELLE MABUMBA** aliuliza:-

(a) Je, Sekta ya Madini imechangia kwa kiwango gani uchumi wa Taifa katika kipindi cha miaka minane (8) iliyopita kuanzia 2005-2012?

(b) Je, ni mikataba mingapi imeingiwa na Serikali katika sekta hii na ni kampuni zipi zilihusika?

(c) Je, ni ajira ngapi zimepatikana kutokana na uwekezaji kwenye Sekta hii ya Madini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sylvester Maselle Mabumba, Mbunge wa Dole, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka nane iliyopita, kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka 2012, kumekuwepo na ongezeko la mchango wa Sekta ya Madini katika uchumi wa Taifa, hususan Pato la Taifa (*GDP*) na mchango wa mauzo ya nje. Katika kipindi hicho mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa kwa kutumia bei za kila mwaka umekua kutoka asilimia 2.9 mwaka 2005, hadi asilimia 3.5 mwaka 2012. Aidha, kwa kipindi hicho mchango wa Sekta ya Madini kwa mauzo nje ya nchi umekua kwa wastani wa asilimia 40.3 kila mwaka.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005 hadi mwaka 2012, Serikali iliingia mkataba mmoja (1) wa uendelezaji wa mgodi wa dhahabu wa Buzwagi, Wilayani Kahama mwaka 2007. Mgodi huo unamilikiwa na kampuni ya *Pangea Minerals Limited*, kampuni tanzu ya *African Barrick Gold (ABG).*

Kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 2010, mikataba ya uendelezaji wa miradi ya madini huingiwa endapo mmiliki ataomba kuingia mkataba na Serikali na iwapo gharama za uwekezaji katika mradi husika hazipungui dola za Marekani milioni 100.

Uendelezaji na usimamizi wa Sekta ya Madini hufanywa kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 2010, ambapo uingiaji wa mikataba ya hiari ya mwekezaji na pia ni lazima mwekezaji awe ametimiza vigezo vilivyoainishwa kwenye sheria hiyo (hususan, kiwango cha uwekezaji).

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya jitihada kuhakikisha kuwa wafanyakazi wazawa wa migodi mikubwa wanalipwa kulingana na taaluma zao sambamba na watumishi wageni katika vyeo vinavyofanana. Aidha, Serikali inaendelea kuyasimamia na kuyalinda maslahi ya watumishi wazalendo.

Katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2012, kumekuwepo na ongezeko la ajira nchini kupitia uwekezaji unaofanywa katika sekta hii ambapo ajira za wazawa

katika migodi mikubwa imeongezeka kutoka 2,077 mwaka 2005 hadi 13,000 mwaka 2012.

**MHE. SYLVESTER MASELLE MABUMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote niipongeze Serikali kwa majibu yake mazuri kwenye sekta hii, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa Watanzania wengi hawajaridhishwa na mchango wa sekta hii ya madini, napenda kujua ni kampuni ngapi ambazo zimefutiwa mikataba yake kwa vile kampuni hizo hazikutimiza matakwa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, siku hizi kumejitokeza wimbi la mauaji na kuvamiwa kwa wafanyabiashara wa madini hapa nchini, Serikali ina mpango gani wa dharura kudhibiti hali hiyo ili wafanyabiashara hawa wa madini wafanye biashara hii na kuchangia uchumi wa nchi yetu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, Serikali imeweza kufuta mgodi mmoja ambao ni wa Kiwira na kuurudisha Serikalini baada ya Mwekezaji kushindwa, lakini swali hili linahitaji majibu ya kina ningeomba Mbunge atupe muda tuweze kumwandalia majibu sahihi na ya uhakika zaidi ili tuweze kutoa majibu ambayo siyo ya ubabaishaji.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la usalama kwenye migodi, yametokea matukio ya vifo vya Wachimbaji maeneo mbalimbali ya nchi, lakini pia imetokea mauaji ya wafanyabiashara wa madini katika Mkoa wa Arusha.

Serikali iliingilia matatizo haya na kukaa kikao na wafanyabiashara wa madini na wachimbaji wadogo wa Mkoa wa Arusha, kikao hicho nilifanya mimi mwenyewe na kukumbushana majukumu yetu wote katika kulinda usalama katika maeneo yetu ya kazi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kikao kile wafanyabiashara na wachimbaji wa madini, Mkoa wa Arusha na pote nchini ambako tulikuwa na kikao Jumapili iliyopita, tumekubaliana wote kuweka kipaumbele cha usalama kwanza katika shughuli za madini kabla ya kufanya shughuli zingine.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa kumekuwa na maswali mengi sana kuhusiana na mikataba inayoingiwa na Serikali na kwa kuwa maswali haya yanajitokeza kwa sababu ya kukosekana *transparency* (uwazi). Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu sasa mikataba yote ya Serikali iidhinishwe na Bunge kabla haijasainiwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, tutakumbuka kwamba Tanzania pia ni mwanachama wa *forum* ya Kimataifa ambayo inasimamia uwazi katika Sekta hii ya Madini

ambayo kwetu hapa ni maarufu kama (*TEIT*), lakini pia mikataba hii siyo kwamba ni ya siri, mikataba hii ipo wazi kama Mbunge au mwananchi yeyote anataka kuiona, zipo taratibu za kupitia kuweza kuiona mikataba hii.

Mikataba itakayofuata tunashirikiana na Kamati zinazohusika za sekta husika katika kuipitia na kushauriana na inafanywa kwa uwazi kabisa. Kwa hiyo, ushauri alioutoa Mheshimiwa Mbunge kwamba iletwe ipitishwe na Bunge, tutaufikiria na pale tutakapoona inafaa, basi tutafanya hivyo.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika nashukuru. Kwa kuwa, ajira nyingi katika migodi hii hasa migodi ya dhahabu, vijana wenye elimu kidogo ya ufundi wanahitajika na kwa kuwa, katika Wilaya ya Kahama ambako kuna migodi miwili mikubwa ya dhahabu kwa maana ya Buzwagi na Bulyankhulu**,** Wilaya ambayo haina Chuo chochote cha Ufudi. Je, Serikali inawaambia nini vijana wa Wilaya ya Kahama ambao wapo pale kushuhudia watumishi wanatoka nje ya Wilaya na hasa nje ya Mkoa wa Shinyanga? Naomba majibu.

**SPIKA:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Waziri wa Elimu, kwa kifupi.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, Serikali ina azma ya kujenga Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi nchi nzima kama ambavyo tumeahidi na mpango tumeuandaa. Hivi sasa tumegawa

kazi hiyo katika mafungu matatu. Sina hakika sasa hivi kwa ghafla Kahama ipo katika fungu lipi, ama fungu la kwanza ama la pili ama la tatu, lakini nitakuwa tayari kumpatia Mheshimiwa Mbunge baada ya kikao hiki.

**SPIKA:** Sawa, hili swali ni *too specific*. Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu atauliza swali hilo.

Na. 5

**Sheria ya Ardhi Kutoendana na Matakwa ya Sheria ya Madini**

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU** aliuliza:-

Sheria ya Madini ya mwaka 2010 inaelekeza pamoja na mambo mengine kuhakikisha kuwa wananchi wanaopisha ujenzi wa migodi mipya wanafidiwa, wanajengewa makazi mapya yaliyo bora na kuhamashiwa huko kabla ya mradi wowote mkubwa wa uchimbaji madini haujaanza; lakini utekelezaji wa matakwa hayo ya sheria unahitaji sheria ya ardhi irekebishwe ili kuweza kutekeleza hayo:-

Je, ni lini Serikali itarekebisha Sheria ya Ardhi ili iendane na matakwa ya Sheria ya Madini kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanaopisha migodi wananufaika ipasavyo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, kwa jitihada zake za kufuatilia haki za wananchi wote wa Tanzania. Namshukuru sana kwa mawazo yake mazuri na ya kizalendo. Pili, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa upungufu alioueleza Mheshimiwa Dkt. Kafumu ulikwishabainishwa na Serikali na umeanza kufanyiwa kazi kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imeandaa rasimu ya Muswada wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini ambapo rasimu ya sheria imekamilika na inategemewa kuwa itawasilishwa Bungeni katika Mkutano wa 14 baada ya kuridhiwa na Serikali.

(b) Aidha, Serikali imeanza mchakato wa kuzifanyia marekebisho sheria zinazokinzana na dhana ya uthamini wa mali zikiwemo Sheria za Ardhi na Sheria ya Madini ili ziendane na mabadiliko yaliyopo sasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeunda Kamati ya Watalaam kwa ajili ya kufanya uchambuzi wa sheria

zinazokinzana katika uthamini wa mali zikiwemo Sheria ya Ardhi ya 1999, Sheria ya Madini ya 2010, Sheria ya Utwaaji Ardhi ya 1967 na Sheria za Kodi ili kubainisha hoja zitakazozingatiwa katika marekebisho ya sheria hizo.

Kamati hiyo inajumuisha watalaam kutoka Ofisi ya Rais Ikulu, Ofisi ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara ya Maji, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maliasili na Utalii na Sekta Binafsi. Pia, hatua za kumwajiri mtalaam mshauri kwa ajili ya kazi hiyo zimeanza.

Kutokana na umuhimu wa marekebisho kwenye Sheria za Ardhi, kazi hiyo itapewa kipaumbele ili mapendekezo ya marekebisho hayo yaweze kuwasilishwa katika Bunge lako Tukufu ifikapo Februari, 2014.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika nakushukuru. Pia namshukuru sana Waziri kwa majibu yanayoridhisha, lakini nina swali moja dogo la nyongeza. Katika orodha ya Watalaam watakaoshiriki kwenye kuchambua sheria hizi naona Wizara ya Nishati na Madini haihusiki, hii ni lazima ihusike kwa sababu Wizara hii inahusika na uvunaji wa rasilimali kutoka ardhini. Ningependa kujua ni kwa nini Serikali haijahusisha Wizara hii katika timu ya watalaam? Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante, Naibu Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, itakuwa ni kughafirika kwa Ofisi katika kuandaa jibu hili, vinginevyo Wizara ya Nishati na Madini itajumuishwa kwenye Kamati hiyo, kwa maana ya kwamba sasa hivi wanashiriki, wapo tayari kwenye Kamati hiyo.

**MHE. GAUNDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Wilayani Mbinga, Kijiji cha Mdundualo kuna machimbo ya makaa ya mawe na wale wananchi walihamishwa hata kabla ya kulipwa fidia, Serikali imekiri kwamba hizi sheria zinakinzana. Je, hawa wananchi watashughulikiwaje na Serikali katika muktadha huu?

**SPIKA:** Mheshimiwa swali lako mwishoni linasemaje, kwamba wananchi wamefanyaje?

**MHE. GAUNDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, hawa wananchi ambao wamehamishwa kabla ya kulipwa fidia watashughulikiwaje wakati Serikali yenyewe inakubali kwamba sheria zinakinzana ili waweze kupata haki yao ya kujengewa nyumba?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nifafanue kwamba, ni kweli kama Mheshimiwa alivyosema katika swali la nyongeza kwamba, kuna sehemu nyingine ambapo katika Sekta yetu ya Madini katika utekelezaji wananchi kweli kwa bahati mbaya walihamishwa bila kuwa wamepata fidia.

Suala hili sasa hivi tunashughulikia na Sheria yenyewe ya Madini, Kifungu cha 56 kinaruhusu kabisa kwamba wananchi wanapohamishwa wawe wanapewa fidia na pia kuhamishwa ili kusudi waingie kwenye makazi mbadala. Suala hili tunalishughulikia na Profesa Muhongo, kwa hiyo ni kitu ambacho tunakitambua.

Mheshimiwa Spika, niombe tu kwamba, wale ambao wana wananchi walio katika hali hiyo watuletee taarifa. Ahsante.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika nakushukuru. Mimi nitakuwa na swali dogo tu. Pamoja na upungufu wote ulioainishwa kwa wakazi wa Nyamongo wanaopisha mgodi wa *North Mara,* wamekuwa wakilalamikia sana kuhusu fidia wanayopewa. Walikuja wakaonana na Mheshimiwa Waziri, hususan kuhusiana na *Task Force* iliyoundwa, wanataka wapewe utaratibu ule wa zamani. Kwa hiyo, nilitaka nijue, Mheshimiwa Waziri amefikia wapi? Kwa sababu wanapinga hiyo *Task Force* kwa kuwa inawapa fidia ambayo siyo na wanalazimishwa, wakati mwingine hata wanabomolewa, wengine wanawekwa mpaka Magerezani. Nilitaka kauli ya Mheshimiwa Waziri.

**SPIKA:** Karibu tutamwita Mheshimiwa Esther, Mheshimiwa wa Nyamongo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri kwamba, ni kweli Kamati ile walikuja kuwawakilisha wananchi na nilikutana nao na pale pale nilitoa maagizo kwa Kiongozi wa Kamati ile ambayo tulituma kwenda kushughulikia uhakiki na niliagiza kwamba, basi wakishakamilisha kazi ile walete taarifa kwangu ili niweze kutolea maamuzi. Kwa hiyo, ile taarifa itakapokuwa imewasilishwa, basi tutamshirikisha Mheshimiwa Mbunge. Nashukuru sana.

Na. 6

**Ukusanyaji wa Kodi za Majengo Jijini Dar es Salaam**

**MHE. MUSSA A. ZUNGU** aliuliza:-

Kodi za majengo kwa sasa katika Mkoa wa Dar es Salaam hukusanywa na *TRA,* lakini tangu chombo hicho kikabidhiwe jukumu hilo, bado hakijaonesha mafanikio; na kutokana na hali hiyo, Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam zimejiandaa vizuri katika kuleta mabadiliko ya kukusanya kodi wenyewe:-

Je, Serikali iko tayari kuratibisha jukumu hilo kwa Halmashauri za Jiji?

**NAIBU WAZIRI FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Marekebisho ya Sheria ya Fedha, yaani *The Financial Laws Miscellaneous Amendment Act* ya 2008, ilikasimu kwa Mamlaka ya Mapato ya Tanzania *(TRA)* jukumu la kukusanya kodi ya majengo kama Wakala kwa niaba ya Halmashauri za Serikali za Mitaa. Kama ilivyoelezwa kwenye Sheria, hatua hii ilichukuliwa kwa lengo la kuboresha makusanyo ya mapato yatokanayo na kodi ya majengo na pia kuwajengea uwezo watumishi wa Serikali za Mitaa katika ukusanyaji wa kodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa, *TRA* wamepewa jukumu la kuthamini, kukadiria, kukusanya na kuhesabu, na kuhasibu kodi ya majengo. Sheria imeruhusu *TRA* kukusanya kodi ya majengo kwa niaba ya Serikali za Mitaa kwa muda wa miaka mitano kuanzia Julai, 2008 hadi Juni, 2013. Tangu *TRA* ilipokabidhiwa jukumu la kukusanya kodi ya majengo, ilifanikiwa kuongeza jumla ya makusanyo kwa Halmashauri zote tatu za Mkoa wa Dar es Salaam kwa kiasi cha Shilingi milioni 3,891.13 kwa miaka mitatu ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 41.42. Viwango vya ongezeko kwenye makusanyo vinatofautiana na kila Halmashauri kama ifuatavyo:-

Kinondoni asilimia 30.07, Ilala asilimia 41.81 na Temeke asilimia 72.82. Ongezeko hili ni kwa kutumia wigo wa kodi

uliokuwepo mwaka 2008 pamoja na bajeti zilizokuwa zikiandaliwa na Manispaa zenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sheria za Ukusanyaji wa Kodi ya Majengo zilifanyiwa marekebisho ili kuiwezesha *TRA* kukusanya kodi hiyo kwa muda wa miaka mitano ambayo imekwisha Julai, 2013, Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa inatarajiwa kuleta mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Kuziwezesha Halmashauri kukusanya kodi hiyo tena. Mapendekezo haya yatafanyika kwa wakati na kuwasilishwa ili ipitishwe na Bunge lako Tukufu.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kujua tu, kwa takwimu alizoonesha Mheshimiwa Waziri, zimeonesha tu ongezeko la asilimia 10 mpaka 11 kwa Halmashauri zote katika Mkoa wa Dar es Salaam ambazo bado kwa uwezo na nafasi ya *TRA* ni ndogo sana. Je, ni changamoto zipi ambazo zimefanywa na *TRA* na wao kuweza kukwama na kukusanya kwa kiwango hicho kidogo tu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Manispaa ya Ilala imejiwekea malengo sasa ya kukusanya Shilingi bilioni tisa kutokana na majengo mengi makubwa kukua katika Mji huu wa Ilala na Mji wa Dar es Salaam; na kwa vile Sheria sasa imepitwa na wakati, na *TRA* hukusanya mapato yake kwa mujibu wa Sheria, ni *commitment* ipi ambayo Serikali

inatoa hapa Bungeni kuwa Sheria hii sasa iletwe hapa kufanyiwa marekebisho ili Halmashauri hizi sasa ziweze kukusanya mapato haya? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ambayo inaikabili *TRA* katika kukusanya mapato haya kwa kiwango ambacho kingetegemewa, kwanza kulikuwa na uhusiano na masuala ya ile misingi ya kuthamini majengo yenyewe. Msingi huu ulikuwa wa viwango vilivyokuwa vimewekwa, vilivyoanzishwa mwaka 2002. Kwa hali hiyo, *TRA* wakawa wanakusanya mapato kidogo sana ukilinganisha na hali halisi kwa sababu viwango vya mwaka 2002 ya soko la majengo siyo sawa na vya mwaka 2008 au 2013. Kwa hiyo, kwa hali hiyo, kufuatana na *base* waliyokuwa wanaitumia ikabidi wakusanye mapato pungufu zaidi.

Vile vile kulikuwa na changamoto ambayo inatokana na jinsi gani ambavyo majengo yamethaminiwa. Siyo majengo yote yalikuwa yamethaminiwa. Kwa hali hiyo, *TRA* walikuwa wanawajibika kukusanya pale tu ambako kwanza jengo limethaminiwa, lakini vile vile ile *bill* imepelekwa kwa mteja. Kwa hiyo, kulikuwa na suala vile vile la taarifa la kujua mteja yupi yuko wapi, kwa maana ya anwani kamili, majina kamili ya wale wahusika wanaotakiwa kutozwa kodi hiyo. Kwa hiyo, kulikuwa kuna changamoto kadhaa ambazo ziliathiri zoezi zima kwa upande wa *TRA*.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye swali la pili, kama nilivyojibu katika swali la msingi, ni kwamba Serikali tayari

inafanya utaratibu ili Manispaa za Dar es Salaam zile tatu, na Manispaa nyingine saba ambazo zimeainishwa katika mradi maalum wa mambo ya *mass valuations* na *property tax* ziweze kurudishiwa mamlaka yake yenyewe kujikusanyia. Hii inafanya: kwanza, kwa kutoa mafunzo maalum au kutoa uwezo wa kutosha kwa Manispaa hizi kukusanya wenyewe kodi ya mapato. Kwa hiyo, hii ni jambo ambalo tayari Serikali inalifanyia kazi na siyo muda mrefu sasa Manispaa hizi zitaendelea kukusanya mapato yake yenyewe.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sitta!

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali inajitahidi kuja na njia mbadala za kukusanya kodi, lakini naomba nitoe uzoefu wangu niliyoupata mimi mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, siku mbili kabla sijaja hapa Bungeni, nilikwenda kulipia *Road License* kwenye Mtaa wa Samora. Wakanieleza kwamba sasa hivi kuna utaratibu mpya unaoitwa Max Malipo. Nikaenda kulipia nje kwa msichana ambaye amekaa kwenye kiti fulani hivi, tukajikuta kama watu 10 tunasubiri Max Malipo. Kwa bahati mbaya yule msichana akatuambia hana salio. Tukaenda kituo cha pili, hivyo hivyo tukaambiwa hakuna salio. Tulikuwa wengi tu! Wakasema na nyinyi Wabunge wenyewe mwone Sheria nyingine mnazopitisha huko. Mimi nikarudi nyumbani na

fedha. Kesho yake nikamtuma dereva tena akalipie *Road License,* naye akanitumia *message,* ninayo mpaka sasa hivi kwenye simu, ananiambia mtandao hakuna, nimerudi na hela.

Sasa nikafikiria, kama ndiyo utaratibu mpya ambao unakusudiwa kuimarisha ukusanyaji wa kodi, mimi na wenzangu wangapi tumerudi nyumbani bila kulipa kodi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuiuliza Serikali: Je, haioni kuna umuhimu wa kuendelea na utaratibu wa zamani wa kulipa kodi wakati njia nyingine zikiimarishwa? Tunapoteza fedha kiasi gani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Naibu Waziri naomba majibu.

**NAIBU WAZIRI FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba nasikitika kuwa limetokea hili jambo. Kwa kweli maana nzima ya kuweka njia mbadala za kukusanya mapato ni kuongeza ufanisi. Sasa kama kwa bahati mbaya haikutokea hivyo, basi nikiri kuwa itabidi tulipitie, tuliangalie na tuangalie hiyo sehemu ambayo Mheshimiwa alipata matatizo, kulikuwa kuna *issue* gani? Kwa hali hiyo, siwezi kutoa jibu la moja kwa moja. Lakini tutafuatilia kwa makini na sisi wenyewe tutaongea na *TRA* kuangalia kuwa: Je, hizi njia ambazo wao waliziweka mbadala, zinasaidia?

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kifupi, ni kweli kuwa *TRA* peke yake, vile vituo vyake havitoshelezi na ndiyo maana kukawa kuna haja ya kutaka ku-*speed up.* Sasa na sisi tutaangalia basi ili tuzidi kuboresha badala ya kuleta usumbufu kwa wateja. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa sababu sisi tuna *interest* ya kukusanya mapato, tunaomba taarifa hii itolewe ndani ya Bunge hili. Taarifa ya haya aliyosema Mama Sitta yarudishwe humu Bungeni kabla hatujaondoka. *(Makofi)*

Tunaendelea na swali linalofuata na Mheshimiwa Selemani Bungara atauliza swali hilo.

Na. 7

**Upungufu wa Walimu, Vitabu vya Kufundishia**

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA** aliuliza:-

Upungufu wa Walimu, vitabu vya kufundishia, maabara na mazingira magumu ni mambo ambayo yamelalamikiwa na Watanzania wengi kwa huduma za elimu hasa sekondari, hali iliyosababisha hata matokeo ya Kidato cha Nne mwaka huu kuwa mabaya sana.

(a) Je, Serikali haioni kuwa haya ni matokeo ya upungufu huo uliolalamikiwa kila siku?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na tatizo hilo?

(c) Je, Serikali haioni kuwa hali hii inaweza kusababisha vijana wengi wasiende shule?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saidi Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ufaulu wa mwanafunzi unachangiwa na mambo mengi ambayo ni pamoja na jitihada ya mwanafunzi mwenyewe, ufuatiliaji na ushirikiano baina ya wazazi ama walezi, jamii na wadau wa shule husika sambamba na upatikanaji wa Walimu, vitabu, Maabara na mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa Walimu, Serikali huajiri na kupanga Walimu wapya wanaohitimu mafunzo ya Ualimu kila mwaka kulingana na uwiano wa mahitaji ya Halmashauri husika ili kukabiliana na changamoto hiyo. Mwaka 2012/2013 jumla ya Walimu wa Sekondari 14,060 wakiwemo Walimu 7,838 wa Shahada na 6,222 wa Stashahada walipangwa katika Halmashauri mbalimbali nchini. Aidha, katika kipindi hicho, Walimu 13,633 wa Shule za Msingi walipangwa nchini na kupata jumla ya Walimu 27,693. Zoezi la ajira na upangaji wa

Walimu ni endelevu mpaka wapatikane Walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mpango wa kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Shule za Sekondari za Serikali za wananchi ili kuzifanya kuwa shule rafiki, yaani *functional schools.* Mpango huo ni pamoja na kujenga miundombinu ya Maabara, vyumba vya madarasa, vyoo na kuweka miundombinu ya maji na umeme kwenye Shule za Sekondari 1,200 ifikapo mwaka 2015. Kati ya shule hizo, shule 264 za awamu ya kwanza tayari zimeanza kujengwa zikiwemo Shule za Sekondari Kivinje na Mbuyuni za Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa. Awamu ya pili itahusisha shule 528 na awamu ya tatu itahusisha shule 408. Aidha, jumla ya vitabu 2,125,580 vikiwemo vya sayansi na hisabati vimeshasambazwa kwenye Shule za Sekondari 3,999 tangu mwaka 2008 hadi 2012.

Mheshimiwa Spika, jitihada hizi za Serikali zinalenga kuhakikisha kuwa shule zinakuwa na mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia ili kuwafanya wanafunzi kupenda kwenda shule kupata stadi na maarifa ambayo yatawafanya kuwa na matokeo mazuri. Hivyo, natoa wito kwa wazazi na walezi na jamii kwa ujumla kuhakikisha kuwa suala la elimu linapewa kipaumbele katika ngazi zote kwa sababu elimu itawawezesha watoto wetu kukabiliana na changamoto mbalimbali za maisha zinazowazunguka.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa jibu zuri la Mheshimiwa Waziri, lakini amekiri kwamba kuna upungufu huo. Je, ili ipatikane elimu bora kwa kila Mtanzania, yeye haoni kwamba inahitajika kasi, ari na nguvu mpya katika jambo hilo? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi, ni kwamba jitihada zinafanyika za Serikali kuhakikisha upungufu huu unamalizika angalau baadhi ya mambo kufikia mwaka 2015 tukawa tumekamilisha, na hasa kwenye Shule za Msingi, fedha za rada tayari zimeshaanza kufanya kazi. Sasa zoezi la kusambaza vitabu linaendelea, na mfumo mzima wa kupeleka madawati kwenye Shule za Msingi kutumia fedha hizo, michakato inaendelea kwa kutumia Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, lakini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ni moja ya Wizara ambazo zimewekwa kwenye mpango wa *Big Results Now (BRA),* yaani Matokeo Makubwa Sasa. Kwa hiyo, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge tutahakikisha jambo hili linakwenda kwa kasi na ari mpya ili mambo ya elimu yaweze kutekelezeka.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Wizara hii ni moja kati ya Wizara sita zilizopewa vipaumbele, nilitaka kujua tu, wana mpango gani kuhakikisha kwamba Wakaguzi wa Elimu wanaboreshewa mazingira yao? Kwa sababu wakaguzi hawa ni muhimu sana katika kuboresha elimu hapa nchini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, moja ya vipengele au mambo tisa ambayo *Big Results Now* kupitia Wizara ya Elimu tunatekeleza ni pamoja na kuwezesha Idara ya Ukaguzi iweze kutembelea Shule za Msingi na Sekondari. Kwa hiyo, suala hili tunalithamini na sasa hivi tuko kwenye mchakato wa Idara hii ya Ukaguzi kuwa Mamlaka ili iweze kufanya kazi vizuri. Kwa hiyo, tunatambua suala la Idara ya Ukaguzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa Serikali imejitahidi sana kupeleka Walimu na mara nyingi Walimu wengi wanapenda kuishia Mijini: Je, Serikali sasa imejipanga vipi kuhakikisha inapeleka Walimu wa kutosha katika maeneo ambayo yana uhaba mkubwa sana wa Walimu hasa vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli baadhi ya Walimu

wanapangwa, lakini wengi wanaishia Mijini. Lakini suala hilo kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), yupo hapa anatusikia, tutashirikiana katika kulikabili.

Mheshimiwa Spika, hata katika kupanga Walimu, mimi na Mheshimiwa Waziri wangu Dkt. Shukuru Kawambwa tumepanga mfumo kwamba tunapopanga Walimu tunahakikisha *first priority* ni kuwapeleka Walimu kwenye Halmashauri zile zenye mazingira magumu ili Walimu wote waweze kufika huko vijijini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbatia, swali la nyongeza.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri kwenye majibu yake amesema fedha za rada zaidi ya Shilingi bilioni 55 zitatumika kwenye vitabu nakala milioni 18 na kwa kuwa vitabu hivi havijafanyiwa uhariri wa kutosha na ukapelekea kuvunjwa kwa *EMAC* tarehe 5 mwezi wa Sita mwaka huu 2013 siku ya Jumatano hapa Bungeni: Je, Wizara haioni ni busara kuunda chombo au Chama cha Wahariri wa Vitabu ili vitabu hivi vikitumika viweze kuwafanya Watanzania waweze kufikiri yakinifu?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbatia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vitabu hivi ambavyo tunavinunua kwa pesa za chenji ya rada, tayari Wakandarasi wameshapewa kazi hiyo na wengi wao wameshatimiza kazi ya kupeleka vitabu maeneo husika, kasoro baadhi ya Wazabuni ambao hawajakamilisha kazi hii tutajitahidi tuhakikishe kwamba, wanakamilisha mapema. *EMAC* tumeivunja na tunatengeneza taratibu nyingine ya chombo ambacho kitasimamia vifaa vya kufundishia ikiwa ni pamoja na vitabu, ambacho kitafanya kazi vizuri zaidi kushinda iliyokuwa *EMAC.*

**SPIKA:** Haya, tunaendelea. Siku nyingine muwe mnaongea huko nje, maana maswali ni haya haya na majibu ni haya haya kila siku.

Sasa tunaendelea Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, atauliza swali hilo.

Na. 8

**Uwekezaji Katika Sekta ya Uvuvi**

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO** aliuliza:-

Tanzania imebarikiwa kuwa na Bahari, Mito na Maziwa yenye vivutio, matumbawe na samaki wa aina nyingi:-

(a) Je, kwa nini Serikali imeshindwa kuwekeza kwenye Sekta ya Uvuvi na kujikosesha mapato yatokanayo na uvuvi?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kuna Mataifa yananufaika kinyume cha Sheria kupitia Bahari, Mito na Maziwa yaliyo Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Mgogoni, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya Sera za Nchi yetu, Serikali ilijitoa katika uwekezaji wa kibiashara na badala yake inahamasisha uwekezaji wenye tija. Hadi sasa jumla ya viwanda 43 vya watu binafsi vinavyochakata samaki na mazao yake vimejengwa hapa nchini. Katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, mazao ya uvuvi yenye thamani ya shilingi bilioni 254.9 yalisafirishwa nje ya nchi. Aidha, Serikali imefanikiwa kupata mrabaha wa shilingi bilioni 6.8 kutokana na usafirishaji wa mazao hayo ya uvuvi katika kipindi hicho.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inadhibiti utoroshaji wa mazao ya uvuvi kwa kutumia mifumo ya kufuatilia meli ya *Vessel Monitoring System* ama *Automatic Information System.* Aidha, Serikali imekuwa ikitumia ushirikiano uliopo

wa Nchi Kikanda kwa kutumia mashirika kama vile Kamisheni ya Tuna ya Bahari ya Hindi *(Indian Ocean Tuna Commission)* na Kamisheni ya Bahari ya Hindi *(Indian Ocean Commission).* Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu ina uwezo wa kuchunguza taarifa za meli zinazovua katika maji yetu kinyume cha Sheria na kuchukua hatua stahili. Katika Mwaka wa Fedha 2012/2013, jumla ya meli za uvuvi za kigeni 36 zilipewa leseni za kuvua katika Bahari Kuu na kuiingizia Serikali, Dola za Kimarekani 1,305,698. Hata hivyo, tunaendelea kujenga uwezo wa Mamlaka kwa kuipatia vitendea kazi na watumishi zaidi ili kuweza kubaini na kuzikamata meli chache ambazo zinavua na kutorosha mazao ya uvuvi kutoka bahari yetu. Vilevile, Wizara ina vituo 21 vya doria vinavyoratibu kwa kushirikiana na wadau wengine ili kudhibiti uvuvi haramu na utoroshaji wa mazao ya uvuvi kwenye Bahari, Maziwa Makuu, Mito, Mabwawa, Mipakani, Viwanja vya Ndege na Bandarini.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kutokana na majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri, imeonekana dhahiri kwamba, Sekta Binafsi imeshindwa kusimamia katika eneo hili. Je, ni lini Serikali itaifanyia marekebisho Sheria hii ili yale maeneo ambayo Sekta Binafsi wameshindwa kuyaendeleza Serikali iyasimamie kwa masilahi ya Taifa?

(ii) Meli iliyoitwa ya "Magufuli" tulipata wafadhili waliosaidia kukamatwa meli ile kutoka Afrika ya Kusini; je, hawa wadau 21 ambao wanadhibiti uvuvi haramu wamefanikiwa kukamata meli ngapi na boti ngapi kutoka nje wakati uvuvi haramu bado unaendelea katika bahari zetu?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sera yetu kwa sasa inavyosisitiza ni kwamba, Serikali iandae mazingira wezeshi, ambayo hii inagusa kwanza; Sheria, Kanuni na Taratibu; pili; mahala ambapo miundombinu ya msingi inahitajika ni jukumu la Serikali. Ila ukija sasa katika uwekezaji ambao ni wa kibiashara, angalau mpaka sasa hatujajiandaa kurudi kule kwa sababu hii ni Sera inayogusa Sekta nyingi za Kiuchumi. Bado kama Serikali, tutaendelea kuandaa mazingira wezeshi na pia kushiriki na Sekta Binafsi chini ya utaratibu wa *PPP,* kuhakikisha kwamba, Sekta Binafsi inakua na inachukua hatamu katika kufanya kazi hiyo ya msingi.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni kwamba, vituo nilivyovitaja vya doria, vimekuwa vinawashika watu wengi na meli kadhaa za ndani na za nje, ikiwemo hiyo ya Magufuli. Pamoja na kwamba, tuliomba msaada kutoka Afrika ya Kusini kutuwezesha kwa vyombo ambavyo hatukuwa navyo, bado kimsingi jukumu hilo lilifanywa na watu wetu wa ndani. Wale walikuja kutoa nguvu, kutushika

mkono, lakini jukumu lilifanywa na watu wetu wenyewe wa ndani kwa ujumla.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Waziri, anajibu swali la msingi alisema kwamba, Serikali imepata mapato ya mrabaha ya asilimia 6.8 na meli ambazo amezitaja zimekusanya mrabaha huo ni 36. Je, Mheshimiwa Waziri anakumbuka aliwahi kusema katika Bunge hili kwamba, wametoa leseni za meli 112 na meli hizo zote ambazo ametoa leseni hakuna hata meli moja ambayo imetozwa mrahaba; haoni Serikali bado haijakuwa makini katika kukusanya mapato yanayotokana na uvuvi wa Bahari Kuu na kwa hiyo, haoni kwamba, ni vyema sasa meli hizi ambazo zinapewa leseni, ili mapato yapatikane wanaopewa leseni watozwe mrabaha baada ya kupewa leseni hata kabla ya kwenda kuvua kama wanavyofanya nchi nyingine ili tuweze kupata mapato ya kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tofauti iliyopo kati ya idadi niliyoitaja hapo nyuma ya 124 na hii ya 36 ni vipindi husika. Maana kama itakuwa umenisikia, kwa hii idadi, nimeongelea kipindi

cha mwaka mmoja tu badala ya kipindi kile nilichotaja kwa meli 124.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kweli nakubaliana na yeye kwamba, kuna meli zilizopewa leseni na mrabaha haujakusanywa kwa meli zote kule nyuma.

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba, Kamati yako ya Kisekta, ilitoa maelekezo maalum na hata Kamati ya Bajeti, ikatoa maelekezo maalum na sasa kama Wizara, tumejipanga na tumeshafanyia kazi taratibu hizo. Kwa hiyo, taarifa tutakayoitoa katika siku za usoni kwa uhakika itaonesha utekelezaji wa maelekezo hayo tuliyopewa na Kamati hizo mbili za Kisekta kutoka hapa Bungeni.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa wavuvi wadogowadogo wanachangia sana katika Uchumi wa Taifa, lakini vilevile lishe bora kwa Wananchi wanyonge inategemea sana upatikanaji wa matumizi ya samaki wadogowadogo kama vile dagaa na vibua. Je, Serikali ina mpango gani sasa kuweka juhudi za makusudi kuweza kuwanyanyua wavuvi wadowadogo ambao hali zao zinazidi kuwa duni kadiri siku zinavyokwenda? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la

Mheshimiwa Dokta Kamani, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane naye kwamba, kweli wavuvi wadogo wanahitaji kuungwa mkono waweze kufanya shughuli yao kwa tija zaidi na kwamba, uvuvi wao mdogomdogo unachangia sana katika lishe na katika Pato la Kaya na Pato la Taifa. Niseme tu kwamba, tayari kuna jitihada zinazofanyika, lakini ni chini ya utaratibu wa mkopo na tayari hivi sasa katika Benki ya *TIB* kumekuwepo na dirisha lenye fursa kwa wakulima wadogowadogo, wafugaji wadogowadogo na wavuvi wadogowadogo kwenda kukopa kule. Tayari kwa upande wa wavuvi wadogowadogo zaidi ya shilingi karibu bilioni moja kwa sasa zimeshakopeshwa na Benki hii.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge hili na kupitia kwa Mheshimiwa mwuliza swali, nitoe tu wito kwa wavuvi wadogowadogo wajiunge katika vikundi na waende zaidi katika taasisi za fedha kukopa kwa sababu nadhani mwelekeo wetu Kisera utaendelea kubaki kuwa ni huo.

Na. 9

## Hali Duni ya Wavuvi Ukanda wa Pwani

**MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU** aliuliza:-

Hali ya wavuvi walio wengi katika Ukanda wa Pwani ni duni sana, kwa sababu ya nyenzo duni na uvuvi wa jadi

wanaofanya usio na tija; lakini kwa sababu Serikali ina mipango mikakati iliyoainishwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011 – 2015):-

Je, ni shughuli gani ambazo Serikali mpaka sasa zimeshaanza kufanyiwa kazi na ni kwa kiwango gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Mohammed Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano kupitia Programu ya kuendeleza Sekta ya Uvuvi, ambayo nayo ni Mpango pia wa Miaka Mitano (2012/2013 hadi 2016/2017). Mpango huu umeainisha nyanja kuu tano za kuendeleza sekta ambazo ni kuboresha ubora na viwango vya mazao ya uvuvi, kuimarisha ukuzaji wa viumbe kwenye maji, kuimarisha shughuli za utafiti, mafunzo na ugani, kupitia na kuboresha Sera, Sheria na Kanuni za Uvuvi na Mashirikiano ya Kisekta katika masuala mtambuka.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Programu hii na Mpango huo, Serikali imetekeleza kazi zifuatazo katika Ukanda wa Pwani:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mradi wa *MACEMP,* imetumia jumla ya shilingi 6,702,865,484 kuwawezesha wavuvi wadogo, ambapo jumla ya miradi 470 ikiwemo Miradi 220 ya Uvuvi, ambayo iliwanufaisha Wananchi 8,082. Pia, Serikali imekarabati Kituo cha Ujenzi wa Boti kilichoko Mtwara – Mikindani, kwa ajili ya kutoa mafunzo ya uvuvi na utengenezaji wa zana za wavuvi wadogo na imejenga mialo mitatu ya kisasa ya kupokelea samaki katika Wilaya za Rufiji, Mafia na Kilwa ili kusaidia wavuvi wadogo kupata soko la uhakika. Vilevile, wavuvi wamehamasishwa kuanzisha vikundi ambapo hadi sasa jumla ya *VICOBA* 124 vimeanzishwa katika Wilaya za Kilwa vikundi 38, Mafia vikundi 63 na Rufiji vikundi 27.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ukuzaji Viumbe kwenye maji Ukanda wa Pwani kupitia Mradi wa *MACEMP,* bado Serikali imewapatia Wananchi mafunzo katika nyanja mbalimbali ambazo ni ukuzaji viumbe kwenye maji chumvi watu 741 wamepata mafunzo, ukuzaji lulu kwenye chaza watu 87, majaribio ya kufuga samaki aina ya perege kwenye maji chumvi watu 56, kilimo cha mwani 38, kuongeza thamani ya zao la mwani kwa kutengeneza sabuni kutokana na mwani watu 26 wamepata mafunzo. Aidha, vituo vya ufugaji samaki vya Mtama – Lindi na Mbegani – Bagamoyo, vimepatiwa vitendea kazi ili kuongeza uzalishaji wa vifaranga vya samaki.

**MHE. AMINA MOHAMMED MWIDAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa idadi ya wavuvi Tanzania ni zaidi ya milioni mbili; na kwa takwimu alizotoa Mheshimiwa Naibu Waziri hapa inaonesha wazi kuwa ni idadi ndogo sana ya wavuvi ambao wamefaidika na Mradi huu wa *MACEMP;* ni kama asilimia 0.4 au chini ya hapo. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutuletea Bungeni tathmini ya utekelezaji wa Mradi huu na mafanikio yake?

(ii) Kwa kuwa *MACEMP* imemaliza muda wake sasa hivi; na Miradi mingi ya Serikali ambayo inapata ufadhili ikimaliza muda wake nayo inajifia. Je, Serikali ina mpango gani wa kuuendeleza Mradi huu uwe endelevu?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mwidau, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja; ndiyo, nipo tayari kuandaa taarifa kamili na kuiwasilisha hapa ama kumpatia yeye Mbunge, juu ya utekelezaji wa huu Mradi wa *MACEMP.* Kama mwanzo ni Mradi uliofanikiwa, umekuwa na changamoto zake, lakini pia tumejifunza mambo ya kuboresha. Pamoja na kwamba, Mradi wenyewe kama huu wa *MACEMP* umeisha, mwingine umeanza chini ya jina la Mradi wa *Smart Fish,* unaofanya kazi karibu sawa na zile zilizofanywa na *MACEMP,* lakini tutaandaa taarifa na kuileta hapa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kama nilivyosema, tayari tuna mpango tulioutaja tena hapa katika kuwasilisha bajeti yetu ya Kiwizara, miezi michache iliyopita na huo Mradi unabainisha zaidi kwamba, nafasi yetu kama Serikali ni ipi na wadau nao taratibu ni zipi. Kwa kuwa wameshashiriki katika vikao vingi vya kuendeleza na kuandaa mpango huo wa Kisekta, mpango huu utafadhiliwa kwa kiasi kikubwa na Serikali na kwa uhakika tunatarajia utakuwa endelevu na kama Mradi wa *MACEMP* ulionekana mdogo, tunakiri, lakini unaanza mahali, unapojifunza unazidi kupanua na kuboresha na kuhakikisha kwamba, wanufaika watakuwa wengi zaidi.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa ukuaji wa Sekta ya Uvuvi Ulimwenguni unajielekeza sasa katika ufugaji wa samaki; na kwa kuwa nchi zilizoendelea katika ufugaji wa samaki zimefanikiwa kwa kuanzisha maeneo maalum ya ufugaji wa samaki kama inavyofanyika katika maeneo maalum ya viwanda. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutuma Wataalamu wake kuja katika Wilaya ya Mkinga, kufanya utafiti wa eneo linalofaa tuweze kuanzisha *Fish Park* katika Wilaya ya Mkinga?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la

Mheshimiwa Kitandula, Mbunge wa Mkinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na yeye kwamba, *future* ya uvuvi zaidi ni kwenye ukuzaji viumbe kwenye maji ama *Fish Farming* na kwamba, tumeshabainisha maeneo tayari ya kuendeleza sana ufugaji wa viumbe kwenye maji. Ukanda wote wa Pwani ni kati ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, niseme tu mwitikio wa watu katika maeneo mengi umekuwa mzuri na tupo tayari kuja kwenye Jimbo lake, Wilaya ya Mkinga. Tutawatuma Wataalamu washirikiane na Uongozi wa Wilaya, kujaribu kubainisha na kuwa na mpango utakaofanya kazi na utakaosimamiwa na Halmashauri na Wadau katika eneo hilo, tukishirikiana na Wilaya.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nchi yetu inakabiliana na tatizo kubwa la utapiamlo kwa watoto na akina mama na hasa wajawazito lakini nchi hii inakabiliwa pia na tatizo kubwa la ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu nguvu zote katika sekta hii ya uvuvi zimeelekezwa kwenye bahari na maziwa lakini tumeona faida hakuna. Nchi hii ina mito mingi sana na mabonde mazuri ya kuweza kufuga samaki. Naomba kuiuliza Serikali, haioni sasa imefika wakati, tunapotenga fedha kwa ajili ya maendeleo ya vijana kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na tunapotenga

fedha kupitia Wizara hii ya Uvuvi na Mifugo, wangeunganisha nguvu pamoja ili kuanza sasa kufungua miradi mikubwa ya ufugaji wa samaki kwa vijana na hasa katika Jimbo la Peramiho ili kuondoa tatizo hili la ajira. Je, Serikali inaweza kujibu kwamba mpango huu sasa ni wakati wake muafaka na inaweza kuuanza haraka sana?

**SPIKA:** Haya, swali la nyongeza refu, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuunganisha nguvu ni mkakati mzuri na kwa sasa chini ya utaratibu wa *Big Results Now,* lengo ni hilo la kuhakikisha kwamba kinachopangwa kinatekelezwa kwa kushirikisha wadau wa kila sekta japo walengwa watakuwa ni makundi ya vijana, akina mama na na watu wetu katika vijiji ili kuweza kuhakikisha kwamba uratibu umeboreshwa kwa matokeo makubwa sasa. Nakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, nadhani kwa kipindi kitakachokuja, kwa uhakika lengo ni hilo na tunatarajia kwamba Bunge litatuwezesha kuendeleza mipango hiyo ya *Big Results Now* ili kutambua manufaa kwa sasa.

Na. 10

## Wanafunzi Wanaojiunga na Mafunzo ya JKT

**MHE. JOSEPH R. SELASINI** aliuliza:-

Wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita na vyuo hutakiwa kujiunga na mafunzo ya JKT:-

(a) Je, ni asilimia ngapi ya wanafunzi wanaojiunga na Jeshi kwa mwaka ikilinganishwa na idadi ya wale waliotakiwa kujiunga?

(b) Je, kati ya wanafunzi wanaojiunga na JKT, ni wangapi wanatoka kwenye vyuo vya Serikali na wangapi kwenye shule/vyuo binafsi?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kurejesha mafunzo kwa mujibu wa Sheria kwa vijana waliomaliza kidato cha sita. Mafunzo hayo yameanza mwaka 2013 ambapo vijana 41,341 wanatarajiwa kuhudhuria mafunzo. Katika awamu ya kwanza vijana 5,000 (12%) walihudhuria mafunzo kwa muda wa miezi mitatu kuanzia mwezi Machi 2013 hadi Juni 2013. Katika awamu ya pili iliyoanza mwezi Juni, JKT ilichukua vijana 10,000 (24%) na wanatarajiwa kumaliza mafunzo yao mwezi Septemba 2013. Katika awamu ya tatu itakayoanza mwezi Oktoba 2013, JKT itachukua vijana 15,000 (37%) na katika awamu ya mwisho yaani ya nne JKT itachukua vijana 11,341 (27%) mwanzoni mwa Januari na vijana hao watamaliza mafunzo mwezi

Aprili, 2014. Kwa maana hiyo, asilimia halisi na sahihi kwa vijana wote watakaohudhuria mafunzo haya kwa awamu zote nne itapatikana mwishoni mwa mwezi Aprili mwaka ujao.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa limepokea majina ya vijana wa kujiunga na JKT kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Wizara ya Elimu ilipotuletea majina ya vijana hawa, haikutenganisha kati ya vijana wanaotoka katika shule za Serikali na binafsi. Kwa hivyo, sio rahisi kwa Wizara yangu kujua vijana wangapi wanatoka shule za Serikali na wangapi wanatoka shule binafsi. Hata hivyo, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa shule zote za Serikali na watu binafsi za Tanzania Bara zimetoa vijana wa kujiunga na JKT.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, hapo awali mafunzo ya JKT yalidumu kwa mwaka mmoja ambapo vijana walikuwa wakipata mafundisho ya kijeshi na mafunzo ya ujasiriamali na elimu ya kujitegemea. Nataka kujua, katika muda huu wa sasa wa miezi mitatu, ni programu zipi ambazo Serikali au Jeshi limeandaa ili kuwasaidia vijana hawa wanapomaliza Jeshi waweze kupata stadi za kuweza kujiajiri?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Jeshi lina mkakati gani wa kuwafuatilia hawa vijana baada ya mafunzo kuona kama mafunzo waliyopata hawayatumii kwa njia za kihalifu ili waweze kuyatumia katika njia iliyo sahihi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa ni kweli hapo zamani yalikuwa yanatolewa mafunzo ya mwaka mmoja, mafunzo ambayo yanalenga mafunzo ya kijeshi pamoja na ujasiriamali lakini mpaka sasa katika kipindi hiki ambacho tuna matatizo mbalimbali ya kifedha, hatukuweza kutekeleza jambo hilo lakini bado dhamira hiyo ya kufundisha vijana mafunzo ya kijeshi na mafunzo ya ujasiriamali, basi mafunzo hayo bado yanaendelea na tutafanya kila linalowezekana ili tuhakikishe mafunzo hayo yanatolewa katika kiwango kinachohitajika.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tuna mkakati gani katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania kuwafuatilia vijana hawa ambao tumekuwa tukiwapa mafunzo ya kijeshi. Kwa kawaida, hakuna utaratibu huo maalum lakini nafikiri ni ushauri mzuri, kuanzia sasa, sisi Wizara ya Ulinzi pamoja na Jeshi la Ulinzi, tutafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba tunafuatilia vijana hawa ili tuweze kujua kwamba baada ya mafunzo kwa jinsi gani wanatumia mafunzo haya ili wasiyatumie katika kufanya vitendo vya uhalifu, nafikiri ni ushauri mzuri, tutauzingatia.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa ni nia njema ya Serikali ya kuwapeleka vijana wanaotoka *form six* na wale wa vyuo katika mafunzo ya JKT lakini toka kuanzishwa kwa mafunzo haya tunajua kwamba idadi inaongezeka na changamoto za miundombinu zimekuwa ni kubwa hasa kwa makazi ya wakufunzi pamoja

na suala zima la nishati ya umeme katika baadhi ya kambi kama Bulombola, Mkoani Kigoma. Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba inaondoa kero hii katika vikosi vya JKT ili vijana wetu waweze kupata mafunzo muafaka?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Jafo kwamba mahitaji ya vijana ambao wanajiunga na JKT kila mwaka yanaongezeka. Kila mwaka tunaendelea kupokea idadi kubwa sana ya vijana na kwa maana hiyo mahitaji mbalimbali ya miundombinu na kadhalika nayo yameongezeka.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikiendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba Wizara yangu inatengewa fedha za kutosha ili iweze kukidhi mahitaji ya vijana ikiwemo ujenzi wa mabweni ya uhakika pamoja na nyumba za wakufunzi kwa kadiri inavyowezekana.

Kwa hiyo, napenda tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuifanya kazi hiyo na kuwahimiza Wizara ya Fedha ijitahidi kadiri inavyowezekana kutupatia fedha ya kutosha ili tuweze kutekeleza wajibu huo.

Na 11

**Barabara ya Kolandoto – Sibiti na Daraja la Mto wa Sibiti**

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA** aliuliza:-

(a) Je, ni lini ujenzi wa barabara ya kutoka Kolandoto kupitia Mwanhuzi – Meatu – Mto Sibiti utaanza?

(b) Je, ujenzi wa daraja la Mto Sibiti umefikia hatua gani ya utekelezaji?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulukwa, Mbunge wa Meatu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kolandoto kupitia Mwanhuzi - Meatu – Mto Sibiti – Oldeani *Junction* (km 328), ni barabara kuu na imeainishwa katika mpango wa utekelezaji wa kazi za Wizara katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014 ambapo kazi iliyopangwa kufanyika ni upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Jumla ya shilingi milioni 500 zimetengwa katika mwaka 2013/2014 kwa ajili ya kazi hiyo. Taratibu za manunuzi za kumpata Mhandisi Mshauri atakayefanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea. Aidha, mpango wa ujenzi wa barabara hiyo utaanza baada ya kukamilika kwa usanifu

wa kina na kupatikana kwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa daraja la Mto Sibiti umeanza ambapo Serikali kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* iliwekeana saini na kampuni ya *'Hainan International Ltd'* toka China kwa ajili ya ujenzi wa daraja hili na maingilio ya barabara zake tarehe 7/8/2012 kwa gharama ya shilingi za Kitanzania 19,236,729,905/=. Mradi unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia 100. Aidha, Mhandisi Mshauri anayesimamia kazi hii ni *Intercontinental Consultants and Technocrats Pvt Ltd.* ya India ikishirikiana na *M/S Apex Engineering Co. Ltd* ya Tanzania. Hatua iliyofikiwa ni uwekaji wa nguzo za msingi *(piles)* wa daraja hilo. Aidha, kazi ya kusafisha eneo la mradi imekamilika.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Barabara hii itakapopita katika mji wa Mwanhuzi- Meatu itaathiri wananchi ambapo nyumba nyingi zitabomolewa ikiwa ni pamoja na majengo ya Serikali. Kwa bahati mbaya sana, *TANROADS* walipofika pale Meatu, Mwanhuzi, hawakuwasiliana na Halmashauri angalau kukubaliana barabara ipite sehemu gani ili kuepuka ile athari ya kutoa fidia kubwa kwenye majengo yatakayobomolewa. Je, Serikali kupitia *TANROADS* sasa iko tayari kwenda Meatu na kuwasiliana na Halmashauri ya Meatu ili kukubaliana

barabara ipitie sehemu gani ili kupisha mji, kuepuka gharama za kubomoa pamoja na ulipaji wa fidia kubwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusu daraja la Mto Sibiti, je, litakamilika na kuanza kutumika lini?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa kwa Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, katika jibu letu la msingi, tumeeleza kwamba katika bajeti ya mwaka huu zimetengwa shilingi milioni mia tano kwa ajili ya kuanza kufanya *feasibility study* na *detail design*. *Consultant* wa kufanya kazi hii atateuliwa katika bajeti ya mwaka huu 2012/2013. Sasa, kujua barabara itapita wapi au nyumba zipi zitabomolewa au hazitabomolewa, tusubiri *consultant* atakapomaliza kazi yake, hapo ndipo tutajua ni nyumba zipi katika mji wa Mwanhuzi na maeneo mengine ambazo *either* zitakuwa ndani ya *road reserve* au zitakuwa nje ya *road reserve* kwa mujibu wa Sheria Na. 13 ya mwaka 2007 ambayo ilipitishwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa daraja la Mto Sibiti ambalo linajengwa kwa gharama ya shilingi bilioni 19.236, mkataba ni wa miezi kumi na nane. Kwa hiyo, baada ya miezi kumi na nane daraja hili litakamilika. Serikali iliamua

kujenga kwanza daraja ili ujenzi wa barabara hii yote ya kilomita mia tatu na kitu iweze kukamilika kikamilifu kwa kujengwa kwa kiwango cha lami.

Na. 12

## Utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Vijiji Kumi (10)

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA (K.n.y. MHE. MICHAEL L. LAIZER)** aliuliza:-

Tatizo la maji ni kubwa sana katika Wilaya ya Longido licha ya ahadi ya Serikali kutekeleza mradi wa maji wa vijiji 10 na sasa umepunguzwa kuwa vijiji vitano (5) tu.

Je, ni lini utekelezaji wa mradi huo utaanza?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Jimbo la Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la upatikanaji wa maji lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido. Ili kutatua tatizo hili, Serikali inatekeleza miradi ya maji katika vijiji 10, miradi yenye kuleta matokeo ya haraka pamoja na ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kutoa maji kutoka mlima Meru hadi Longido. Vijiji 10 vilivyopewa kipaumbele ni Irkaswa, Engikareti, Longido, Mairouwa, Les Mundarara,

Sinya, Tingatinga/Ngereyani, Kiseriani, Gelai Bomba na Luondoluo.

Mheshimiwa Spika, hatua za utekelezaji katika vijiji hivyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kijiji cha Longido kipo katika hatua za mwisho za ujenzi wa mradi;

(ii) Vijiji vya Sinya na Les Mundarara vipo katika hatua za kupata wakandarasi wa ujenzi;

(iii) Vijiji vya Irkaswa, Luondoluo, Gelai Bomba na Tingatinga, Halmashauri inapitia makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa miradi ya maji; na

(iv) Vijiji vya Mairouwa, Kiseriani na Engikareti mtaalamu mshauri anaendelea kukamilisha usanifu wa miradi.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Juni 2013, Halmashauri ya Wilaya ya Longido imepokea shilingi bilioni 1.98 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji kupitia programu ya maendeleo ya sekta ya maji. Aidha, kwa mwaka 2013/2014, shilingi milioni 737 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika vijiji 10 na shilingi bilioni 1.143 kwa ajili ya ujenzi wa miradi yenye kuleta matokeo ya haraka katika vijiji vya Matale A, Orbomba na Olchoronyok.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuwapatia maji wananchi wa mji wa Longido kutoka chanzo cha Emurututu kilichopo kwenye mlima Meru. Katika bajeti ya mwaka 2012/2013, Halmashauri ya Wilaya ya Longido imepewa kiasi cha shilingi milioni 450 na inaendelea na taratibu za kupata mtaalamu mshauri atakayefanya usanifu wa mradi. Mradi utakapokamilika utahudumia wananchi wa mji wa Longido na vijiji vitakavyoainishwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha na Longido.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kwa kuwa hatua ya Serikali ya kutenga shilingi milioni 450 ili kumpata mtaalamu mshauri wa kuweza kusanifu mradi utakaoleta ukombozi kwa Wilaya ya Longido kwa kuvuta maji kutoka mlima Meru maeneo ya Emurututu kwenda Longido, ni dhamira njema ya Serikali kwa nia ya kuwasaidia wale wananchi.

Je, Serikali itatenga lini sera ya kutekeleza mradi huo ambako ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi wa Longido?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Longido ni miongoni mwa maeneo yaliyopo kwenye nyanda kame hatua iliyopelekea vijiji 12 vya mradi huo wa maji vijijini

kupata maji tu katika visima vitano tu na vingine maji yalikosekana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba Wilaya zilizoko kwenye nyanda kame zinawekewa mpango mahsusi utakaowezesha kupata maji ili wananchi hawa waweze kushughulika na mambo mengine ya maendeleo badala ya hali ilivyo sasa ya wananchi kuhangaika kutafuta maji usiku kucha na mchana wote? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru kwa kutambua nia njema ya Serikali ya kutatua tazizo la maji katika wananchi wa Longido wa kutoa maji kutoka mlima Meru. Ndiyo maana baada ya kuona kwamba juhudi za kupata maji kwa kutumia visima katika Wilaya ya Longido zilishindikana Serikali ikaamua sasa uamuzi wa kutoa maji kutoka mlima Meru na pale pana chanzo kizuri ambacho kinatoa maji lita 21 kwa sekunde, kwa hiyo ni maji ya kutosha ama lita 75,600 kwa saa.

Mheshimiwa Spika, sasa ni lini mpango huu utaanza kutekelezwa, tumeanza kutekeleza, hatua ya kwanza ni lazima usanifu ukamilishwe, kwa hiyo baada ya hizi milioni 450 ambazo sasa hivi wako kwenye taratibu za kumpata mtaalam mshauri yaani *consultant,* akikamilisha kazi ile, tutaingiza kwenye bajeti ya 2014/2015 ili mradi huu utekelezwe.

Nimetembelea pale, nimemwambia Mkurugenzi wa Halmashauri afanye kinachowezekana kumpata mtaalamu mshauri mzuri na afanye mapema ili ikifikia mwezi wa kumi, wa kumi na moja tunapoanza mzunguko wa bajeti tuwe tumeshapata hayo matokeo tuingize kwenye mpango wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwamba hizi Wilaya zenye matatizo ya maji, tuna mpango gani, tumeshaanza kwa sababu katika Mkoa wa Arusha tumeanza na Wilaya mbili zenye shida ambazo ni Longido na Monduli kwa kuzitengea fedha za kuleta matokeo ya haraka kwa kutumia mabwawa yaliyopo ili kusambaza maji kwa wananchi.

Kwa hiyo, tuna hakika baada ya awamu hii tutaingiza na Simanjiro ambapo tutahakikisha kwamba wananchi wanapata maji kwa teknolojia nafuu ikiwemo ya ujenzi wa mabwawa.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Tatizo la maji nchini tumekuwa tukililalamikia kila siku hapa Bungeni lakini miongoni mwa bahati ambayo Taifa letu tunalo ni kuwa na vyanzo vya uhakika vya maji hususani maziwa kama Victoria, Tanganyika, Rukwa lililoko Jimboni kwangu pamoja na Nyasa. Ni kwa nini sasa Serikali imekuwa ikiwekeza zaidi kwenye visima badala ya kwenda kwenye vyanzo vya uhakika ambavyo vinaweza vikasaidia Taifa zima kuondoa hii kero ya maji? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imekuwa ikiangalia teknolojia mbalimbali ili kutatua tatizo la maji kwa wananchi na ieleweke wazi pale ambapo kuna uwezekano wa kupata maji ya kisima, kwanza ni nafuu kwa maana ya upelekaji miundombinu, kisima hakiwi mbali lakini tunapokuwa na vyanzo vya maji kama mito au maziwa maana yake unaingia gharama kubwa za kusafirisha haya maji kutoka hiyo sehemu lakini pale sasa tunapogundua kwamba uwezekano wa kupata maji kwa njia nafuu kama ya visima haipo, ndiyo tunaamua sasa kutumia teknolojia za maziwa na mito.

Mheshimiwa Spika, nafahamu anaongelea kuhusu matatizo ya maji katika Wilaya yake, mji wa Tunduma. Walishaongelea hapa kwamba wanafikiri wangetoa maji kutoka Ziwa Rukwa, tukakubaliana kwamba sasa hivi vyanzo vilivyopo vya pale vinatosha kutosheleza maji kwa ajili ya wananchi wa Tunduma hapo baadaye tutatoka zaidi ya hapo na kutumia ziwa Rukwa.

Na. 13

**Hitaji la Maji Safi na Salama Nyang'hwale**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR (K.n.y. MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuwapatia maji safi na salama wananchi wa Wilaya mpya ya Nyang'hwale?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula, Mbunge Viti Maalium, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mradi wa maji kwenye vijiji 10 kwa kila Halmashauri. Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale iliyopo Mkoani Geita, inatekeleza miradi ya maji katika vijiji vya Nyamtukuza, Bukwaimba, Izunya, Nyarubele, Kitongo, Ikangala, Kakora, Kayenze na Kharumwa ambao ni Mji Mkuu wa Wilaya ya Nyang'hwale.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji na vituo 10 vya kuchotea maji unaendelea katika kijiji cha Nyamtukuza ambacho kilipata maji ya kutosha. Kwa vijiji ambavyo vilipata maji kidogo vya Ikangala, Kakora, Kharumwa na vijiji vilivyokosa maji vya Bukwimba, Nyarubele na Kitongo, Serikali itatumia chanzo cha Ziwa Victoria kuwapatia maji wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa mtaalamu mshauri anaendelea kufanya upembuzi yakinifu, usanifu, kuandaa michoro ya kiufundi na makabrasha ya zabuni. Kwa mujibu wa mkataba, kazi hiyo inategemewa kukamilika mwezi Septemba 2013. Kwa vijiji vya Izunya na Kayenze, Halmashauri inatafuta mtaalamu mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu, usanifu na uchimbaji wa visima kwa ajili ya kuhudumia vijiji hivyo. Katika mwaka 2013/2014,

Halmashauri ya Nyang'wale imetengewa kiasi cha shilingi milioni 567.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa mradi wa maji wa kijiji cha Nyang'wale unaendelea ukihusisha kufunga pampu ya umeme na kukarabati vituo 15 vya kuchotea maji. Mradi huu utagharimu shilingi milioni 75 ambapo kati ya hizo, shilingi milioni 45 zitatoka kwenye ruzuku ya Halmashauri na shilingi milioni 30 ni kutoka kwenye bakaa ya mwaka 2012/2013. Mradi huu utakapokamilika, utatoa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi 6,665.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuishukuru Serikali kwa kuitengea Halmashauri ya Nyang'wale shilingi milioni 567.5 kwa ajili ya suala la maji.

(i) Je, ni lini sasa pampu hii ya umeme ambayo itafungwa ya Nyamtukuza itaanza kufungwa?

(ii) Visima hivi ambavyo vimetajwa hapa, asilimia 98 havitoi maji. Je, Waziri yuko tayari baada ya Bunge hili kufunga safari na mimi kwenda kuthibitisha visima hivyo kama vimechimbwa kweli na vinatoa maji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Maswali ya Mheshimiwa Amar ni mazuri, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali yote mawili kwa pamoja, nitafanya ziara na niko tayari kwenda na yeye ili nikaangalie kasi ya ufungaji wa pampu na visima hivyo ambavyo havitoi maji ili tuweze kuagizana kwenye *site* nini cha kufanya.

**SPIKA:** Maswali *direct* na mazuri, Mheshimiwa Mwaiposa nafikiri utauliza hivyohivyo.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi. Pamoja na Serikali kutambua tatizo kubwa la maji nchini na kwa kupitia *DAWASA* imejaribu sana kuchimba visima virefu lakini visima vingi nchini ambavyo vimechimbwa bado havijamalizika vikiwemo visima vinne vya Jimbo la Ukonga. Je, Serikali au Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kuwaambia wananchi kwamba ni lini visima hivyo vitamalizika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imechimba visima vingi na hasa Dar es Salaam vimechimbwa vingi na *DAWASA* na vingi vimeonekana havifanyi kazi. Tumeshapata orodha ya visima vyote na tumeagiza *DAWASA* vile visima ambavyo matatizo yake ni madogo kama kuharibikiwa pampu vianze kutengenezwa. Kwa hapa siwezi kusema kama vitaanza lini, nilichukue tu kwa maana kwamba tutaenda kufuatilia na kuona kwamba vinatoa maji mapema ili wananchi wapate maji.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha. Jana kwa sababu moja au nyingine tulishindwa kufanya

kazi yetu ya kupata *briefing* ya kawaida kabla ya kuanza vikao vya Bunge. Kwa hiyo, napenda tukiahirishe kikao sasa hivi twende kwenye ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya kazi hiyo ya *briefing* halafu baadaye mchana *party caucas* wakipenda wanaweza kuendelea na vikao vyao. Sasa hivi twende kwenye *briefing* halafu baadaye *party caucus* kwa utaratibu wao wanaweza kuendelea. Maana yake ni kwamba hatutakuwa na Bunge mchana wote wa leo. Kwa hiyo, naahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 4.45 Asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 28 Agosti, 2013, Saa Tatu Asubuhi)*